LVEMP II Mradi wa Asasi Angalizi za Kijamii

Uganda Coalition for Sustainable Development

SUSTAINABLE ENVIRONMENTAL DEVELOPMENT WATCH
"Driving Sustainable Processes"

Tanzania Coalition for Sustainable Development

LVEMP II Civil Society Watch project

LVEMP II Mradi wa Asasi Angalizi za Kijamiini mradi wa miaka mitatu chini ya Mtandao Angalizi wa Uendelevu wa Afrika Mashariki ambao unatekelezwa kuanzia mwezi Novemba 2011 hadi mwezi Oktoba 2014, kwa ufadhili wa serikali ya Sweden. Mradi huu unatekelezwa kwa ushirikiano wa taasisi za Muungano wa Maendeleo Endelevu wa Uganda (UCSD), Muungano wa Maendeleo Endelevu Tanzania (TCSD), na Mtandao Angalizi wa Mazingira Endelevu wa Kenya (SusWatch Kenya).

Sekretarieti ya Kikanda ya mradi wa SusWatch inahifadhiwa na UCSD iliyoko mjini Kampala, Uganda. Mradi huu ambao ulianzishwa mwaka 2005, unalenga kuhamasisha taasisi za jamii katika ukanda wa Afrika Mashariki kusisitiza juu ya uwajibikaji miongoni mwa serikali na taasisi za maendeleo za kimataifa ili kuakikisha dunia endelevu katika maswala ya kijamii na kimazingira.

Mamlaka ya Mradi huu ni kufuatilia na kuhamasisha utekelezaji wa majukumu ya kitaifa na kikanda katika mikataba ya kimataifa na mipango mingineyo kwa ajili ya maendeleo endelevu katika ukanda wa Afrika Mashariki.

Malengo ya Makuu ya Mradi

Mradi huu unalenga kushawishi na kuhamasisha utambuziwa mfumo wa utendaji unaolenga matokeo (result-based perfomance) katika mradi wa Usimamizi wa Mazingira ya Ziwa Victoria (LIVEMP II) pamoja na utekelezaji wa sera ya Afrika Mashariki juu ya Masuala ya Mabadiliko ya Tabia nchi (EACCP). Kwa upande wa LVEMP II, mradi unalenga
kusimamia shughuli za LVEMPII katika ngazi ya kitaifa na kikanda.

Kipengele I (Ngazi ya kikanda)

Kuimarisha uwezo wa taasisi katika kusimamia vyanzo vya maji na samaki ambavyo vinatumiwa na wadau wa nchi zote (kwa kuzingatia zaidi uoanishaji wa sera, sheria, na viwango vya usimamizi.

Kipengele I (Ngazi ya kikanda)

Kuimarisha uwezo wa taasisi katika kusimamia vyanzo vya maji na samaki ambavyo vinatumiwa na wadau wa nchi zote (kwa kuzingatia zaidi uoanishaji wa sera, sheria, na viwango vya usimamizi.

Malengo Mahususi ya Mradi ni kama ifuatavyo:

• Ufuatiliaji wa mara kwa mara wa utekelezaji wa LVEMP II APL1 (awamu ya kwanza ya LVEMP II) ili kuhakikisha utekelezaji muhafaka wa miradi saba yenye tarehe ya maagano ya utekelezaji (dated implementation convenants)

• Kutathimini mara kwa mara na kuandika uzoefu wa wadau, uwezo, uelewa na kiwango cha kutekeleza mipango ya uhifadhi endelevu wa ardhi (SLM) chini ya mradi wa LVEMP II, katika maeneo teule ya Mto Nyando (Kenya), Mto Simiyu (Tanzania) na Mto Katonga (Uganda), ambavyo vinatokana na miradi ya maendeleo inayotokana na jamii zenyewe yenye lengo la kupunguza vyanzo visivo rasmi vya uchavuzi wa mazingira ya ziwa Victoria na hivo kuboresha utekeleza wa mradi huo wa LVEMPII.

• Kushawishi utekelezaji wa Sera ya Afrika Mashariki ya mabadiliko ya tabia nchi (EACCP), Mashariti ya LVEMPII, mashariti ya LVBC, mashariti ya LVFO na pia mashariti na shughuli za taasisi nyingine za kikanda, kuanzia na tathimini ya ufanisi katika sekta muhimu za maji, kilimo na usalama wa chakula, na upatikanaji wa nishati vijijini.

• Kuimarisha zaidi uwezo wa kitaasisi wa mtandao wa EA SusWatch ili uwe kama mtandao wa kanda wa kijamii ambao unasaidia usiamamizi wa pamoja wa mazingira na maliasili. Pia uwezo huu utausaidia mtandao kufanya kazi za ushawishi na usimamizi wa mradi wa LVEMP II pamoja na mikakati mingine katika Bonde la Ziwa Victoria.

Shughuli kuu za Mradi

• Kufuatilia na kuandika mafanikio katika utekelezaji wa miradi ya saba ijulikanayo kama mradi wa maagano chini ya Mkataba wa makubaliano dhidi ya GEF na EAC pamoja na Mkataba wa kifedha dhida ya IDA na serikali za, Kenya, Tanzania na Uganda.

• Kuandaa warsha kwa ajili ya kushirikishana na kujadili matokeo baina ya watunga sera wa LVEMP II na watekelezaji.

• Kuandaa na kushirikishana tafiti za ufuatiliaji ili kuchunguza mabadiliko katika hali za kimazingira yanayoweza kuonekana wazi wazi, ushiriki wa jamii na mitizamo wao juu ya miradi iliyobuniwa na wanajamii wenyewe.

• Kuandaa mikutano kwa ajili ya taasisi za kijamii na vyombo vya habari kwa ajili ya kukuza ufahamu na kuendeleza upashanaji wa habari kutoka kwenye mradi juu ya LVEMP II na masuala ya mabadiliko ya tabianchi katika ukanda wa ziwa Victoria kwakutumia vyombo na nyezo za kijamii za upashanaji habari.

• Kuandaa majarida ya mara kwa mara na uwekaji pamoja wa habari hizo juu ya tafiti (wa LVEMP II kwa ajili ya taasisi za kijamiii, kama vile mifano ya uboreshaji maisha kutokana SusWatch,kufuatilia Maendeleo ya miradi itokanayo na SusWatch,majarida ya utayari waMabadiliko ya tabia nchi katika LVB, jarida la uchunguzi la Afrika Mashariki, miongoni mwa mengine mengi) ili kutumika kama ushahidi wa kushawishi utekelezaji wa Mradi wa LVEMP II pamoja na kuharakisha utekelezaji wa EACCP (2010).

• Kusajili wa wanachama na kuhimarisha taasisi za mtandao wa EA SusWatch.

Wanaonufaika na Walengwa wa Mradi

• Wanaonufaika na walengwa wakuu wa mradi huu ni zile jamii zenye hali ngumu ya rasilimali katika ukanda wa ziwa Victoria (LVB) ambao umelengwa na Mradi wa LVEMP II.

• Walengwa wengine ni yale makundi yanayotekeleza miradi ya LVBC, LVEMP II yaliyopo nchini Uganda, Kenya, Tanzania, LVFO na EALA.

• NGOs / asasi za kiraia na vyombo vya habari vyenye nia na mradi huu ambavo vinafanya kazi na vina uhusiano na jamii lengwa za mradi wa LVB katika maswala kila siku.
Hasa hasa, mashirika yasiyo ya kiserikali na asasi za kiraia zitanufaika kutokana na kuimarishwa kwa uwezo wao katika ujuzi wa elimu, utetezi na ushawishi unaohusiana na mtandao wa maendeleo endelevu katika ngazi ya kikanda. EA SusWatch kwa namna nyingine, itazihusisha asasi za kiraia na mitandao ya Rwanda na Burundi katika baadhi ya shughuri hasa ikizingatiwa kwamba Rwanda na Burundi zimejiunga na LVEMPII chini ya APL2 tangu Juni 14, 2011.

Utekelezaji wa Mradi wa LVEMP II CS Watch

Mradi huu ni wa kikanda ambao uko chini ya uhifadhi wa mtandao wa Sus Watch wa Afrika Mashariki (ambao unahusisha TCSD, Sus Watch Kenya na UCSD).
Kwa hiyo shughuli za mradi huu zitafanyika kwa namna ya 'umoja' wakati masuala muhimu ya kitaifa yakiachwa yatekelezwe na wahusika washirikia husika kwa niamba ya mtandao kwa kuzingatia mikakati ifuatayo:
• Tathmini zenye ushahidi pamoja na maadalizi ya nyaraka za maendeleo kwa njia ya ripoti mbadala (kama vile majarida ya SusWatch. Kwa mfano, uandaaji wa kujitegemea wa taarifa kutokana na uzoefu katika miradi pamoja na uwekaji pamoja wa

habari hizo (i.e.information packaging) ni aiana mojawapo ambayo miradi inayoendeshwa na jamii husika china ya mradi wa SusWatch maisha ya tafiti (Livelihood case studies) kutoka vyanzo vya maji nchini Uganda (Mto Katonga), Kenya (River Nyando) na Tanzania (Mto Simiyu); Jarida la utayari wa Mabadiliko ya Tabia nchi ndani ya LVB,kifupi kuonyesha kiasi cha utayari kwa ajili ya kukabiliana na changamoto za maendeleo na mabadiliko tabia nchi anda ya LVB (kwa ajili ya maji na usafi wa mazingira, kilimo na usalama wa chakula, nishati vijijini) kama ilivyo kwenye Sera 2010 ya Afrika Mashariki Juu ya mdiliko ya tabia nchi (EACCP)

• Kazi ya Utetezi. Hii inahusisha utoaji na fursa na midahalo katika ngazi za kitaifa na kikanda, kwa ajili ya kubadilishana mawazo na kujadili taarifa ripoti na mapendelezo mbadala

• Kujenga uwezo.Hii ni kupitia njia ya utoaji wa elimu ya miradi husika, mbinu, pamoja na uhimarisha wa taasisi pamoja kuhimarisha mifumo ya ndani ya kitaasisi, rasimali watu n.k, ziara za kubadilishana ujuzi na uzoefu ambazo zinaweza kuchochea kujifunza na kukuza suluhisho za changamoto za maendeleo; pia kusaidia jamii na taasisi za kijamii kuwa na mawasiliano ya mara kwa mara wale wenye mamlaka katika utekelezaji wa mradi wa LVEMP II.

• Kujenga Muungano.Hii itafanyika kwa kuhakikisha kwamba mradi wa EA SusWatch unakuwa karibu zaidi na jamii na taasisi za kijamii zinazofanya kazi katika ukanda wa ziwa Victoria (LVB) katika nchi 3; kuhakikisha uhalisia katika ngazi ya taifa na kikanda, na pia kutambua masuala ya kampeni za kijamii kwa ajili ya kazi za kwa pamoja.

• Ushirikiano na wadau wengine katika Ukanda wa Ziwa Victoria (LVB).Hii itafanyika kwa kuhakikisha ushirikiano miongoni wadau kama vile LVBC, LVFO, vyombo vya habari na wadau wengine kwa lengo la kufanikisha utekelezaji wa mradi wa LVEMP II.

Ni jinsi gani Mradi wa Mradi wa Ungalizi wa Taasisi za Kijamii wa LVEMP II unaratibiwa?

Ukifanya kazi kama mtandao wa uangalizi wa Uendelevu wa Afrika Mashariki, Mradi huu unaundwa na kamati tendaji ya mradi (ambayo inaundwa na watu saba wakiwemo wenyeviti Wenyeviti wa mitandao 3 ya washirika), ambayo inahusika na usimamizi na pamoja na kufanya maamuzi yanayohusu utendaji wa kila siku.

Muungano wa Maendeleo Endelevu wa Uganda (UCSD) ndio taasisi kiongozi ya kikanda ya mradi huu ambayo inaongozwa na mratibu wa Kanda wa Mradi, akisaidiwa na wafanyakazi wengine 3 (afisa habari na mawasiliano wa kanda, Afisa uhamasishaji wa kanda pamoja na afisa fedha na uongozi wa kanda). Pia, kila moja ya mitandao 3 itakuwa na wawakilishi wawili wa kitaifa-waajiriwa (ambao watakuwa ni mratibu taifa na mtunza fedha msaidizi) ambao watafanya kazi chini ya usimamizi wa kamati kuu ya taifa husika.

Matokeo yanayotarajiwa

Uandalizi na upatikanaji wa matokeo endelevu na ya kudumu kutoka katika mradi wa LVEMP II kulingana na malengo (chini ya kipengele teule) kutoka APL1 mpaka APL3 ili kuepuka upotevu wa muda katika feizi hizi.
Upatikanaji wa msukumo kwa ajili ya utekelezaji wa mapendekezo ya sera ya jumuiya ya Afrika Mashariki juu ya mabadiliko ya tabia nchi katika kushughulikia uatarishi unaoongezeka miongoni mwa jamii ziishizo ndani ya bonde la Ziwa Victoria (LVB)
Uimarikaji wa Mtandao wa SusWatch wa Afrika Mashariki na kutambuliwa kama majawapo ya mitandao angalizi ya jamii ambayo inajihusisha kwa karibu sana na uhamasishaji wa usimamizi endelevu wa mazingira na maliasili ndani ya bonde la ziwa Victoria, kupitia ushawishi wa pamoja, na upashanaji wa habari miongoni mwa watendaji wa kikanda na wale wa kitaifa.

Ushiriki wa taasisi za kijamii katika mradi

• Asasi teule za kiraia zinaweza kushiriki katika mafunzo na fursa nyingine za kimaendeleo zinazoratibiwa na mradi

CSOs pia zinaweza kushiriki katika ngazi za kitaifa na kikanda kwa njia ya mtandao kupitia vikundi kazi ambavyo utoa fursa kwa ajili ya kuwashirikisha wanachama, taasisi na watu binafsi wenye nia na mradi. Vikundi hivi uhamasisha upashanaji na ubadilishanaji wa mawazo na mapendekezo katika maeneo yote ya ziwa na pia kutoka katika ngazi ya chini (jamii) kuelekea juu (bottom up). Shughuli hizi usaidiwa na walao mwanachama mmoja kutoka katika kamati tendaji ambaye anasaidiwa na mfanyakazi mmoja wa kanda pamoja na waratibu wa kila nchi.

Kundi 3 za kazi ni:

1. LVEMP II Miradi teule ya Agano: Miradi huu uhimiza katika ngazi ya kikanda usawa na utekelezaji wa wakati wa makubaliano ya kikanda na miradi teule kupitia tathimini zinazofanyika mara kwa mara

2: Sera ya Afrika Mashariki juu yya Mabadiliko ya tabia nchi: Sera hii uhamasisha utoaji kipaumbele kwa shughuri za ustahimilivu ambazo zinapunguza uhatarishi na kuongeza ustahimilivu wa maliasili(hasa katika sekta nyeti za maji, kilimo na chakula, na upatikanaji wa nishati katika maeneo ya vijijini).
3. Mirado ya Maendeleo inayotokana Jamii husika: Miradi hii ulenga kutambua miradi midogomidogo halisia katika Mto Nyando (Kenya, mto Simiyu (Tanzania) na Mto Katonga (Uganda).

Sanduki 1: Muhtasari wa Mradi wa LVEMP II

LVEMP II ni jitihada ya kikanda ya nchi wanachama watano ambao unaratibiwa na Tume ya Bonde la Ziwa V ictoria (LVBC). Mradi huu unafadhiliwa na Benki ya Dunia kupitia Umoja wa Maendeleo ya Kimataifa (IDA) pamoja na mataifa wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki. Vyanzo vingine ni mfuko wa dunia wa kuhifadhi Mazingira (GEF) pamoja na na Sweden. IDA inafadhili ngazi ya Kitaifa, wakati GEF na Sweden ufadhili shughuli za kikanda. Mradi huu wa miaka nane (yaani kuanzia Septemba 2009 hadi Juni 2017) unatekelezwa katika awamu tatu ziulikana kama Adjustable Programu (APL). APL1 ambayo mtandao wa EA SUS Watch unafuatilia zaidi kwa kipindi cha 2009-2013 ambayo inashirikisha nchi za Kenya, Tanzania na Uganda inafadhiliwa na IDA dola milioni 90, Sweden dola milioni 10, GEF dola milioni 7, na Wakopaji dola milioni 7.8

Mradi wa LVEMP II Umeanzishwa ili kukuza na kuendeleza shughuri za Awamu ya kwanza ya LVEMP I (1997 - 2005) kuimarisha uwezo wa taasisi za kikanda na kitaifa katka kusimamia uhifadhi wa rasilimali maji pamoja na kuwekeza katika miradi ya bei nafuu kwa ajili ya kupunguza na kuzui uchafuzi wa maji na mmomonyoko wa udongo.

Mradi huu unatekeleza vipengele/shughuri kuu 4 (ambavyo ni kuimarisha uwezo wa taasisi kwa ajili ya kusimamia rasilimali za maji zinazotumiwa na watumiaji wengi;Uchafuzi wa maji unaotokana na chanzo Fulani; Uhifadhi wa vyanzo vya maji; Uratibu na Usimamizi wa Mradi).

Shughuli hizi zinalega kupunguza matatizo ya kimazingira katika vyanzo vyake (mfano, ndani ya Ziwa, katika ukanda wa pwani na pia kutoka katika bonde) na pia zinatarajiwa kufanya yafuatayo: (a) kuongeza ufanisi wa kiuchumi katika matumizi ya rasilimali zinazoingiliana mipaka ya asili, (b) kuwa na matokeo ya manufaa zaidi kwa nchi katika zilizoko upande wa chini kabisa wa vyanzo hivi vya maji (downstream countries) (c) kuboresha maisha ya jamii zinashiriki katika mradi huu. Maelezo zaidi kutoka: http://www.lvemp2kenyas.org/

Picha: New Vision Uganda

Kwa Mawasiliano:

Uganda Coalition for Sustainable Development UCSD

Mhusika mkuu Kitaifa na Taasi la Kiongozi ya Kanda
Mratibu wa Kanda–Mradi wa Uangalizi wa asasi za kiraia wa LVEMP II wa Mtandao wa Uangalizi wa Uendelevu wa Afrika Mashariki (C / o UCSD) Nsambya - Kabalagala (Gaba Road)
P.O.Box 27551 Kampala (Uganda)
Simu: +256 414 269461
Barua pepe: ugandacoalition@infocom.co.ug

SUSTAINABLE ENVIRONMENTAL DEVELOPMENT WATCH
"Driving Sustainable Processes"

Mhusika mkuu Kitaifa waKenya
Mratibu wa Taifa –Mtandao Angalizi wa Mazingira Endelevu (SusWatch Kenya)
Kisumu, Eneo la Milimani, Mkabala na Palmer Hotel, Nje ya barabara kuu ya Nairobi-Kisumu.
P.O. Box 47146 00100 Nairobi (Kenya)
Simu: +254 721 878329/254 721 3447 07
Barua Pepe: suswatchkenya@gmail.com

C S T D
Tanzania Coalition for Sustainable Development

Mhusika mkuu Kitaifa Tanzania
Mratibu wa Taifa –Muungano wa Maendeleo Endelevu Tanzania (TCSD)
Kitalu namba 1831, Kirumba,mtaa wa Magomeni (Mkabala na Benki ya Azania - Mwanza
P.O. Box 77266, Dar es salaam, TANZANIA
Simu: +255-22-277 1328, Simu ya mkononi +255 731 357121
Barua pepe: tcsd2005@yahoo.co.uk